

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

TABIBU MKUU

(Habari ifuatayo ni hadithi ya mambo ambayo yamenakiliwa katika Mariko 5:24-34, SUV)

Watu wengi walikuwa wamemzingira Yesu wakati alipokuwa akitembea njiani ambako kulijaa vumbi. Wanafunzi wake nao walikuwa wamemzunguka huku wakijaribu kuwa kizingiti kati yake na umati huo ambaa uliendelea kuwasonga. Sauti ya kicheko cha watoto nayo ikasikika wakati watoto wakikimbia huku na huko kati ya umati ule. Nazo sauti za wanawake na wanaume zikasikika wakati wakizungumza na kujadili kuhusu mambo ambayo walikuwa wamejionea. Basi sauti hizo zikazidi kupaa juu kwa ukelele mkubwa. Naye kiwete asiyeweza kutembea kwa haraka kama watu wale wengine akaendelea kufuata umati huo kwa nyuma. Wakati huo huo mama ambaye alikuwa na mtoto mwenye homa kali akafululiza katika njia hiyo huku akijaribu kumfikia Bwana Yesu.

Katikati mwa halaiki hilo kubwa la watu mwanamke mmoja alipenya katikati mwa kwa upole lakini kwa ari isiyotingisika huku akijaribu kumfikia Yesu. Mwanamke huyo alikuwa amefunika uso wake kwa kitambaa, uso ambaa ulikuwa umekunjamana na kuchakaa. Kwa kutumia macho yake ambayo yalikuwa yamebonyeza ndani ya uso wake mwanamke huyo alimtazama Yesu kwa makini, huku mwili wake mnyonge ukijaribu kupenya ili aweze kufika katikati mwa umati huo. Mwanamke huyo alikuwa mngonjwa sana, na damu yake ilikuwa imevunja kwa miaka kumi na miwili! Yeye alikuwa ametumia mali nyingi kwa matabibu na madaktari wengine wa kitaalamu lakini hawakuweza kumsaidia. Basi ikawa kwamba yeye ametumia mali yake yote kwa kutafuta matibabu lakini badala ya kupata nafuu hali yake ya afya ilizidi kuzorota kwa sababu hakukuwa na mwanadamu ambaye angweza kumponya au kumrudishia afya yake.

Lakini siku moja mama huyo akasikia habari kuhusu mwanaume mmoja aliyeitwa Yesu. Akapata kusikia jinsi mtu huyo alikuwa akitembea kutoka kijiji kimoja hadi kingine huku akiponya magonjwa na maradhi yote ya waliokuwa wagonjwa. Hata akasikia jinsi ambavyo mtu huyo alitoa watu mapepo, akafanya viwete kutembea na hata vipovu kupata kuona. Jambo hilo likamfanya mama huyo kuwa na wazo kwamba—“Kwa hakika naonelea kama kwamba mtu huyu wa Mungu ambaye pia ni mwalimu anaweza kuniponya.”

Basi akiwa na tumaini na matarajio makuu mama huyo akaanza kumtafuta Yesu. Lakini hata ingawa sasa amempata Yesu alitambua kwamba Yeye alikuwa mwenye shughuli nyingi na kwamba amezungukwa na watu. Lakini mwanamke huyo akajambia, “Nikiyaguza mavazi yake tu naamini nitapona.” Ndiposa huku akiwa na msukumo wa imani mama huyo alipenya kati ya umati huo na alipokuwa karibu na Yesu akatupa mkono wake na kuunyoosha kumzungukia wanafunzi mmoja wa Yesu na akaweza kuguza mavazi yake Kristo. Mara moja mwili wake ukajaa joto, akapata kuponywa, na kupokea nguvu na uhai mpya.

Basi mwanamke huyo akasimama wima kwa mshangao mkubwa uliojaa utukufu na shukrani. Naye Yesu akasimama na kugeuka huku na huko akiuliza, “Ni nani ameniguza?” Nao wanafunzi wake wakamjibu, “Je! Waona makutano wanavyokusongsangna nawe unasema, Ni nani aliyenigusa?” Lakini Yesu akaendelea kutazama huku na huko kwani alijihisi kwamba nguvu zilikuwa zimemtoka mwilini mwake.

Naye mwanamke huyo akiwa sasa anatetemeka akaijangusha miguuni pake Yesu, na kumweleza kuhusu ugonjwa wake na jinsi alivyopata kuponywa

(Endelea katika Ukurasa 2)



“Nikiyaguza mavazi
yake tu naamini
nitapona.”

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

mara moja. Lakini Yesu huku akiwa ameja upendo na huruma, akamwambia mama huyo, "Binti, imani yako imekuponya, enenda zako kwa amani, uwe mzima, mateso yako yamekwisha."

Kusema kweli njia za Yesu Kristo ni za kushangaza na zimejaa maajabu. Alipokuwa duniani Yesu alifanya muujiza baada ya mwingine wakati ambapo watu waliweka tumaini lao kwake. Watu ambao walikutana na Masihi hawakubaki walivyokuwa hapo mbeleni. Yesu hakuwahudumia watu mahitaji ya kiroho tu bali pia alikutana pia na mahitaji yao ya kihisia na kimwili. Yeye alimfanyia mwanamke huyo kile ambacho wasomi hawangeweza kumfanyia kwani kwa njia ya kiungu aliponya mwili wake na kumrudishia afya yake kwa njia ya muujiza. Kwa kweli wakati huo Yesu ndiye alikuwa Tibabu Mkuu na sisi nasi tunamshukuru Mungu kwa sababu Yeye angali ndiye Tabibu wetu Mkuu.

Kusema kweli kungali kuna nguvu za uponyaji katika wema ulio ndani ya Yesu Kristo. Yeye angali anaendelea kuwahudumia wale ambao wanakuja kwake kwa imani, walio wagonjwa na waliokufa mioyo. Yeye angali katika shughuli ya kuokoa yeyote yule ambaye amefungwa na dhambi, lakini pia Yeye yu tayari kuwahudumia watu ambao wana uchungu wa kihisia na kimwili. Lakini Yesu sio mbadala wa madaktari (wawe wa kimwili au wa kiakili). Yeye ni Mungu wa kweli na mwenye ukubwa wote na ambaye anaweza kufanya hata zaidi ya yale yote ambayo sisi wanadamu tunaweza kufanya. Hakuna lisilowezekana kwa Mungu. Wakati ambapo hakuna tumaini au jawabu, mwangaza na neema yake ya uponyaji wa kiungu unaweza kupenya gizani na kwa njia ya kimujiza uweze kubadilisha hali ya kawaida ya ugonjwa unaomwandama mwanadamu uwe wa kihisia au wa kimwili.

Mwanamke huyo ambaye aliponywa na Yesu alikuwa ametumia wakati wake mwingi, nguvu zake za kimwili, na hata pesa zake nyingi akitafta uponyaji kutokana na ugonjwa aliokuwa nao. Lakini sisi tunao mweke wa kumjua Yesu na hatuna haja ya kungojea au kuchelewa. Tunaweza kuleta shida na mahitaji yetu kwake wakati wowote ule na Yeye anatusubiri kwa upendo ili atufanyie kile ambacho sisi wenyewe hatuwezi kujifanyia. ■



**Kwa maoni ya makusanyiko fulani ya kanisa
kuna wakati ambapo watu huonekana
hawaa imani kwa Mungu kuhusu kuponywa
magonjwa ya kimwili. Je, tunahitaji kuwa na
mwelekeo wa aina gani kwa watu kama hao?**

"Yeye aliye dhaifu wa imani, mkaribisheni, walakin msimhukumu mawazo yake." (Warumi 14:1). Kama Wakristo tunahitaji kuwa tayari kuwashikilia ndugu na dada zetu katika maombi na kuwapenda bila kuwashukumu.

Sauti ya muziki wa kupendeza sana ambayo ishawahi kusikika duniani ni ya watu wa Mungu wakipaza sauti kwa pamoa na kwa nia moja na huku tanakali zao za sauti zikilingana na uimbaji ambao umeimbwa ndani ya Roho.

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwashimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tudembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nydingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kuititia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya jinsi tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@gospeltruth.org

Tahariri



Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu; ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu. —Waefeso 2:6-7

Neema za Bwana Yesu Kristo zingali zamwagika juu yetu hata katika kizazi cha sasa. Je, kuna baraka gani kubwa kiasi hiki kama sisi kibinafsi kuweza kupokea upendo na rehema zake Mwokozi wetu. Somo letu la muhula huu ni uponyaji wa kiungu. Kwa matumizi yake ya kila siku somo hili limeleta mgogoro mkubwa kwa watu wengi katika historia ya kanisa. Lakini toleo hili limepangwa ili kutilia mkazo mafundisho ya biblia bila kujali jinsi ambayo vizazi tofauti vimefundishwa na kuelewa kuhusiana na swala hili. Hata katika Kanisa la Mungu kumekuwa na tofauti ya matumizi na pia ya jinsi ambavyo viwango tofauti vimefundishwa na wahudumu tofauti kuhusiana na swala hili. Vile vile hata katika vizazi tofauti jambo hili limefundishwa kwa njia ilio tofauti. Basi ni jambo muhimu sisi kuhubiri Neno la Mungu na kutambua kwamba Roho Mtakatifu ndiye ataleta uhai na kutuongoza katika njia ambayo Mungu angependa tuishi.

Kuna neema ya uponyaji wa kiungu ambaa ungali unateremka kutoka kwa kiti cha enzi cha Mungu. Kibinafsi, mimi nimetambua kwamba maisha ya imani yana baraka nydingi na faraja nydingi yetu kwenye nyakati za dhoruba za maisha haya. Watu wa Mungu wa kizazi hiki wanaweza kupeana hadithi moja baada ya nyagine ya jinsi Mungu alingilia kati maishani mwao katika hali ya kawaida ya ueneajii wa ugonjwa na maradhi miilini mwao. Hata mimi mwenyewe madaktari waliniambia kwamba ningekuwa kiwete, lakini baada ya miaka mingi ya kuteseka na kupitia mambo mazito Bwana alifanya muujiza mwilini mwangu. Pia mimi mwenyewe nishawahi kuwa chini ya nguvu za Roho na kuona watu wakitolewa mapepo na hata kupata kuponywa. Vile vile, Mungu amefanya miujiza mingi mwilini mwa watoto wangu hivi kwamba hata sina nafasi ya kueleza hayo yote. Basi uponyaji wa kiungu silo jambo la siku zilizopita—ni jambo halisi ambalo lingali kazi hata katika siku hizi zetu.

Jambo la kimsingi kwetu ni sisi kufika mahali pa kumwamini Mungu hivi kwamba haijalishi ni jambo gani litakalotokea, imani yetu ndani ya Mungu haitatingisika. Mimi mwenyewe nishawahi kupitia nyakati za mteso ambako kulionekana kama kwamba Mungu hajibu maombi yangu. Katika nyakati hizo mimi nilimwona Mungu akifanya kazi kwa njia ambazo ilikuwa zaidi ya kimwili. Je, ni kweli kwamba hatuwezi kutumaini hekima yake kama ambavyo tunaweza kutumaini uponyaji wake?

Tunaishi katika kizazi ambacho hakitaki kupatana na mteso na pia hakitaki kungojea. Lakini ili tuweze kumtumikia Mungu kwa njia inayokubalika katika imani ni lazima tufike mahali pa kupata amani inayotokana na mtu kujisalimisha kwa mapenzi na makusudi yake Mungu. Roho wa Mungu atakuwa mwaminifu kuongoza kila mmoja wetu kibinafsi kwenye vipengele vya ukweli. Mtu anahitaji kuwa amekomaa kwa mambo ya kiroho ili aweze kukubali kwamba Roho Mtakatifu anao uwezo wa kufanya kazi, na pia kwamba Yeye atafanya kazi maishani mwa kila mmoja wetu kibinafsi. Lakini pia kutambua kwamba kuna uwezekano wa kuweko tofauti ndogo ya jinsi Roho anafanya kazi katika hali tofauti za watu wake.

Kwa kweli mimi siwezi kuandika miongozo yote ya “kufanya na kutofanya” kuhusiana na swala hili kwa sababu itafika mahali katika msururu wa kuandika miongozo kama hiyo nijipate kwamba nimeingia katika hali ya kutokuwa na unyoofu wa usemi. Niweze kujipata kwamba ninapigia debe mawazo ya mwanadamu, au nidhihirishe viwango tofauti vya kupima mambo, hali ambavyo watu wengi wamejipata wakiwa ndani yake katika nyakati zilizopita. Ukweli ni kwamba sisi tuna mweke mkubwa wa kumwamini Bwana kwa mioyo yetu yote na jambo hilo silo mzigo wa kutufunga. Wakati uponyaji wa kiungu unakuwa kitu cha kumfunga mwanadamu huo ni wakati bora wa mtu kuchunguza maandiko tena na pia kuchunguza uhusiano wake na Mungu.

Bila kusitasita ningw (ya kiungu) kwa kila hali ya maisha yako. Ni kweli kwamba sisi hatuwezi kupata mwokozi bora zaidi, rafiki bora zaidi, na Yeye ambaye atakutana na mahitaji yetu daktari wetu Yesu Kristo. Yule anastahili tuweke imani yetu, kwake.

Michael Smith
April 2018



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujiandikisha na

kupata jarida

za mbele.

Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: Mafundisho ya Uponyaji wa Kiungu

Somo la Biblia: *Bali alijeruhija kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepeotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.* —Isaya 53:4-5

Muhstasari: Moja ya kusudi la Kristo ni kuhudumia mahitaji ya kimwili na kihisia ya wanadamu. Huduma yake pamoja na ile ya mitume ilijaa uponyaji wa magonjwa. Kupitia kwa msalaba wake Yesu alitoa nafasi ya wanadamu kuweza kuponywa milini mwao. Basi kumtumaini Bwana kwa ajili ya uponyaji wetu ni mweke wa ajabu ambao wana wa Mungu wangali wako nao hadi sasa.



I. Unabii Kuhusu Uponyaji Atakaofanya Kristo

- A. Isaya 61:1-2 Yesu alikuja kuleta uponyaji.
- B. Isaya 53:3-5 Alibeba masikitiko na huzuni yetu.
- C. Isaya 35:4-6 Unabii kuhusu miujiza ya Masihi.

II. Uponyaji wa Kristo Duniani

- A. Mathayo 8:16-17 Unabii wa Isaya unatimizwa ndani ya Kristo.
- B. Mathayo 11:4-5 Akaponya vipofu, viwete, wenyewe ukoma, viziwi na hata kufufua wafu (Mathayo 15:30-31).
- C. Mathayo 4:23-24 Akaponya magonjwa na maradhi ya aina yote (Luka 4:40; Luka 7:21).
- D. Matendo 10:38 Akaponya waligandamizwa.
- E. Matendo 2:22 Masihi alidhihirishwa kwa miujiza na ajabu za ishara.

III. Uwezo wa Mitume wa Kuponya Magonjwa

- A. Mathayo 10:1,7-8 Kristo alipatia wanafunzi wake uwezo.
- B. Luka 10:1,9 Wale sabini wakapewa jukumu la kuwponya wagonjwa.
- C. Marko 16:17-20 Neno likadhibitishwa kwa ishara.
- D. Matendo 5:12-16 Mitume wakafanya mambo mengi ya ajabu. (Tazama pia Matendo 6:8; 14:8-20; 19:11-12; 28:8).

IV. Karama ya Uponyaji

- A. 1 Wakorintho 12:4,9 Uponyaji ni karama.
- B. 1 Wakorintho 12:29-31 Watu wote hawajapewa karama ya aina moja.

V. Nguvu za Kristo Hazijabadilika Hata Sasa

- A. Waebrania 13:8 Yesu Kristo ni yeye yule.
- B. Mathayo 28:18 Kristo ana mamlaka yote.

- C. Waefeso 28:8-9 Anao uwezo wa kufanya zaidi ya maombi yetu.

VI. Miongozo kwa ajili ya Wagonjwa (Kuwaita, Kuwapaka Mafuta, Kuwaombea)

- A. Yakobo 5:14-16 Wazee wanatakiwa kuwapaka mafuta wale walio wagonjwa.
- B. Marko 6:12-13 Wanafunzi waliwapaka wagonjwa mafuta.
- C. Matendo 28:8-9 Kuwawekea mikono (Marko 16:18).

VII. Haja ya kuwa na Imani

- A. Marko 11:22 Mwamini Mungu.
- B. Mathayo 13:58 Kutokuwa na imini humzuia Kristo kufanya miujiza.
- C. Mathayo 17:20-21 Imani inayofanya miujiza hutokana na sala na mtu kufunga (kusaumu).

VIII. Umuhimu wa Kumtafuta Mungu

- A. Zaburi 103:2-3 Uponyaji hutoka kwa Mungu.
- B. 2 Mambo ya Nyakati 16:12 Mfalme Asa hakumtafuta Mungu
- C. Mathayo 7:7-11 Ombeni nanyi mtapewa.
- D. 1 Yohana 5:14 Ombeni kulingana na mapenzi yake Mungu.
- E. Waebrania 11:6 Mungu huwapa thawabu wale wamtafutao.
- F. 2 Wakorintho 12:7-9 Mungu haponyi kila wakati watu wanapoomba kuponywa.

IX. Rehema Zake Kristo

- A. Mathayo 14:14 Yesu akawahurumia.
- B. Marko 1:40-43 Yesu amponya mwenye ukoma.
- C. Mathayo 9:35-36 Watu walihitaji mchungaji.
- D. Waebrania 4:15-16 Yesu aguzwa na udhaifu wetu.

Tamati

Basi atukuzwe yeye aezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina. —Waefeso 3:20-21

BARAKA NA MWEKE WA KUPATA

Uponyaji wa Kiungu

“Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenitura kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa.”

Moja ya maandiko yenyeye urembo mwingu ni yale ya Luka 4:18 ambayo Yesu alisoma hadharani kutoka kwa nabii Isaya hapo katika sinagogi kwenye siku ya sabato na kutangaza kusudi na mwito wa huduma yake. Sehemu kubwa kabisa ya huduma ya Kristo ilikuwa



kuponya nafsi za watu kwa njia ya kiroho. Kwa njia ambayo sisi kamwe hatukustahili Kristo alileta neema ya uponyaji kwa nafsi za wanadamu, na kwa njia hiyo akaleta mapatanisho kati ya mwanadamu na Mungu kuitia kwa damu yake ya utakaso. Yule ambaye alikuwa mfungwa akawekwa huru kutokana na dhambi zake, vipofu wa kiroho wakapata kuona, na wale waliokata tamaa wakapata tumaini la kuokolewa.

“Yesu ni mtawala mkuu na angali ana uwezo wa kuponya magonjwa na maradhi ya aina zote.”

katika Isaya 53:4-5: “Hakika ameyachukua masikitiko yetu . . . Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; . . . na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.” Kimuktadha, na kwa njia ya tafsiri, uponyaji huo ultokana na kupigwa kwake na unahusiana na mweke ambao Kristo alitoa ili sisi tupate kuponywa kiroho na kukombolewa nafsi zetu kutoka kwa nguvu za dhambi. Zaidi ya hayo maandiko yanasema kwamba Yesu alichukua masikitiko yetu. Na kwa tafsiri bora neno “masikitiko” linaweza kutafsiriwa kama “magonjwa, maradhi, masumbufo, mateso.” Yeye alitimiza haya yote na pia akatimiza unabii mwininge tofauti ambao ultabiri kuhusu uponyaji ambao angeleta kwa wanadamu wakati ambako macho ya vipofu yangeweza kuona na masikio ya visiwi kuweza kusikia (Isaya 35:4-6).

Kristo Aliponya Wagonjwa

Kuna uwezekano kwamba hatuwezi kabisa kutenganisha huduma ya ya kiroho ya Yesu hapa duniani kutokana na huduma yake ya kuwaponywa watu—kwa maana huduma hizo mbili ziliambatana pamoja. Yesu aliwaambaia wanafunzi wa Yohana Mbatizaji waende kumwambia jinsi

“vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakawwa, viziwi wanasikia, wafu wanaufufuliwa” (Mathayo 11:4-5). Mathayo 8:16-17 inadhibitisha kwa njia ya moja kwa moja kwamba uponyaji wa Kristo kwa miili ya wanadamu ulikuwa wa kutimiza unabii: “Akawaponya wote waliokuwa hawawezi, ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukua magonjwa yetu.” Yesu aliponya magonjwa na maradhi tofauti tofauti (Mathayo 4:23-24) na kuwaponya “wote walioonewa na Ibilisi” (Matendo 10:38). Yeye alionyeshwa kama aliyehitimishwa na kutumwa na Mungu kwa njia ya miujiza, maajabu, na ishara ambazo alifanya mbele za watu (Matendo 2:22).

Wanafunzi Wanaponya Watu

Yesu pia aliwapa wanafunzi wake mamlaka ya “kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina” (Mathayo 10:1). Wale sabini ambao walitumwa kuhubiri injili waliagizwa “waponyeni wagonjwa” (Luka 10:9). Maandiko 5:12 inasema, “Na kwa mikono ya mitume zikafanyika ishara na maajabu mengi katika watu.” Neno la Mungu lilidhibitishwa kwa njia ya ishara ambazo zilifuata mitume wa kanisa la kwanza (Marko 16:17-20).

Karama ya Uponyaji

Karama ya uponyaji ni kipawa cha kiungu ambacho pia kimetolewa kwa kanisa na Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 12:4-9). Hii ni moja ya karama tofauti ambazo Mungu kwa mapenzi yake mwenyewe anaweza kumpatia Mkristo kwa manufaa ya Injili. Karama ya uponyaji kuitia kwa kuwawekelea watu mikono haikutolewa kwa watakatifu wote. 1 Wakorintho 12:29-30 inauliza: “Je! Wote ni mitume? Wote ni manabii? . . . Wote wanatenda miujiza? Wote wana karama za kuponya wagonjwa?” Bila shaka jawabu ya maswali hayo yote ni “la.” Sio wote wana karama ya aina moja, lakini Roho wa Mungu hutoa karama ambazo zinafa kwa mwanadamu na kwa mwili wa waumini kwa wakati unaofaa na katika kizazi cha wakati mmoja.

Hata ingawa kihistoria inaonekana kumekuwa na madhihirisho makubwa ya uponyaji wa ghafla hasa katika nyakati ambapo kanisa liliuhishwa, nguvu kuu za Kristo zingali zafanya kazi katika kizazi hiki chetu. Yeye angali mwokozi wa nafsi zetu na mponyaji wa akili na hata miili yetu. Yesu ni mtawala mkuu na angali ana uwezo wa kuponya magonjwa na maradhi ya aina zote. Waebrania 13:8 inasema, “Yesu Kristo ni yeye

(Endelea katika Ukurasa 6)

yule, jana na leo na hata milele." Naye Yesu akasema, "Nimepewaa mamlaka yote mbinguni na duniani . . . na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:18-20).



"Lakini kusudi la mafundisho hayo hayakuwa yawe ni mzigo wa kuchosha watu bali yalitakiwa kuwa ni nafasi ya sisi kujitoa kabisa kwa Mungu, yule ambaye anatupenda."

kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa. Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kucombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii."

Wagonjwa nao wameagizwa kwa hiari yao na imani yao kuwaita wazee wa kanisa. Wazee hao wanahitaji kufuata mfano wa wanafunzi (Marko 6:12-13) na kuwapaka wagonjwa mafuta. Lakini ukweli ni kwamba nguvu hizo hazitokani na mafuta bali zinatokana na mtu kutii Neno la Mungu. Wazee wanahitaji kuiga mfano wa Kristo na mitume na kuwawekea mikono wagonjwa na kuwaombea (Marko 16:18; Matendo 28:8-9). Kuna baraka na nguvu zinazopatikana kuitia kwa uwekeaji wa mikono, jambo ambalo Mungu analiheshimu linapofanywa na watumishi wake watakatifu.

Mungu Aingilia Kati

Kuna neema ya ajabu ambayo watoto wa Mungu hupewa katika nyakati za magonjwa na mateso. Hata ingawa Wakristo hawajawekwa huru kutokana na magonjwa na maradhi kuna mweke ambao umetolewa wa uponyaji wa mwili kuitia kwa Kristo. Uponyaji wa kiungu sio kitu cha kawaida au kitu kinachotokana na uwezo wa mwanadamu. Uponyaji huo ni wa Mungu kuingilia kati na kubadilisha mambo ya kawaida na kufanya yasiyowezekana kuwezekana. Kumtazama Yesu kwa ajili ya uponyaji wa mwili na kihisia ni mweke ambao umetolewa kwa wana wa Mungu na ni moja ya manufaa ya kumtumikia Bwana. Kusema kweli Mungu tayari ashajidhahirisha kuwa ni mponyaji wa watoto wake katika kizazi hiki.

Miongozo Kuhusu Walio Wagonjwa

Biblia imetoa mwongozo kuhusu wagonjwa katika Yakobo 5:14-16. "Mtu wa kwenu amekuwa hawesi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na

nguvu hizo hazitokani na mafuta bali zinatokana na mtu kutii Neno la Mungu. Wazee wanahitaji kuiga mfano wa Kristo na mitume na kuwawekea mikono wagonjwa na kuwaombea (Marko 16:18; Matendo 28:8-9). Kuna baraka na nguvu zinazopatikana kuitia kwa uwekeaji wa mikono, jambo ambalo Mungu analiheshimu linapofanywa na watumishi wake watakatifu.

Imani Inahitajika

Wakati mwingine watu huponywa kuitia kwa imani ya watu wale wengine; na wakati mwingine wao huponywa kuitia kwa imani yao wenye. Kilicho muhimu na cha lazima ni kwamba—imanu na tumaini la mngonjwa linahitaji kuwa kwa Mungu. Kutokana na kutoamini kwa watu Yesu mwenye hakuweza kufanya miujiza mingi huko Nazareti (Mathayo 13:58). Hata ingawa imani kubwa kama mbegu ya haradali inaweza kusongesha milima, ni jambo muhimu pia kutambua kwamba imani inayotenda miujiza hutokana na maombi na kufunga (Mathayo 17:20-21). Hata ingawa kuna nyakati ambapo Mungu huamua kutowaponya watu, hakuna haja ya imani yetu kutingisika kutokana na jambo hilo, kwa maana lengo la imani hiyo ni kumpata Kristo mwenye, wala si matokeo ya maombi yetu.

Mweke wa Kumtumaini Mungu

Uponyaji wa kweli unatokana na Mungu ambaye "Akuponya magonjwa yako yote" (Zaburi 103:3). Maandiko yanatufundisha kwamba tunahitaji kujenga imani yetu na kumtumaini Mungu kwa mambo yote ambayo yanahusiana na maisha yetu. "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamin kwamba yeze yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao" (Waeranira 11:6). Walio wagonjwa na ambao wanateseka wanahitaji kumtafuta Mungu kwa matarajio ambayo msingi wake ni imani. Katika Agano la Kale Mungu hakupendezwa na Mfalme Asa ambaye alikuwa na ugonjwa miguuni mwake kwa sababu alitafuta uponyaji kutoka kwa matabibu lakini hakumtafuta Bwana kwa ajili ya tatizo hilo (2 Mambo ya Nyakati 16:12). Kwa kweli mtu hastahili kuja kwa Mungu wakati ambapo yeze hana mahali pengine pa kwenda, bali tunahitaji kumjia kama Baba mwenye shauku la kuwapatia watoto wake zawadi nzuri. Kwa watu wengine mafundisho kuhusu uponyaji wa kiungu imekuwa ni msalaba ambao ni mgumu kubeba. Lakini kusudi la mafundisho hayo hayakuwa yawe ni mzigo wa kuchosha watu bali yalitakiwa kuwa ni nafasi ya sisi kujitoa kabisa kwa Mungu, yule ambaye anatupenda. Mtu hupata amani kubwa moyoni mwake hata wakati kuna mashaka ikiwa yeze ameweka imani yake kwa Mwokozi wetu.

Njoo Ukiwa Mwenye Uhakika

Wakati akiwa humu duniani Yesu alihudumia watu waliokuwa wamekufa moyo, na akahudumia wengine kutokana na magonjwa yao ya kimwili. Yesu alifanya hayo kwa sababu aliwaona na "akawahurumia" (Mathayo 14:14). Hata sasa Yesu huchukuana "nasi katika mambo yetu ya udhaifu" (Waeranira 4:15-16). Mtu yejote ambaye yumo gizani katika hisia zake ama katika maumivu ya kimwili anaweza kukaribia kitu cha enzi akiwa na uhakika kwamba atapata nguvu na msaada. Ni baraka na mweke mkubwa ndio ambao tumepewa wa kuweza kumtumaini Masihi kama daktari wetu kwa mambo ya kiroho, ya kimwili, na ya kihisia. ■

Maswali na Majibu

Je, Mungu daima atawaponya watu magonjwa ya kimwili mradi wawe na imani?

Shauku lake Mungu ni kuokoa kila nafsi, na Yeye alitoa ahadi kwamba hatawaacha au kuwaachilia watoto wake.

Lakini Yeye hakuahidi kwamba daima atawaponya magonjwa yote ya kimwili. Katika Maandiko kuna kiwango cha wastani kwa mambo yanayohusiana na swala la mtu kuomba kwa imani, kuamini kwa moyo wake, na pia kujitoa kwa mapenzi yake Mungu.

Mtume Paulo alikuwa na mwiba mwilini mwake (majaribu fulani au mateso ya aina fulani) na yeye akamwomba Mungu kumwondolea mwiba huo. Paulo akaomba mara nyingi.

Lakini jibu la Mungu lilikuwa, "Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu." Mtume Paulo hakuwa na dhambi yoyote na pia hakuwa mkosefu wa imani;

lakini wakati jibu la Mungu lilikuwa "hapana," Paulo naye alijibu vifuatavyo, "Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu . . . Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu" (2 Wakorintho 12:7-10).

Tunahitaji kufanya maombi kulingana na mapenzi yake Mungu kwa imani, huku tukiziamini nguvu zake.

Tunahitaji pia kuomba kwa matarajio lakini pia kwa roho ya kunyenyeka. Wakati Mungu atatupatia jawabu tunahitaji kukubali jibu hilo kwa imani na ujasiri huku tukijua kwamba neema yake itafanya kazi tosha iwe ni katika kupata uponyaji au tukiwa tungali wagonjwa.

Je, kila wakati watu wanapopata magonjwa huwa yametokana na hukumu ya Mungu kwao kwa ajili ya dhambi zao au makosa yao? Je, ugonjwa hutoka kwa Mungu au kwa Shetani?

Magonjwa na maradhi ambayo hupatikana ulimwenguni ni matokeo ya dhambi ambayo ilitendwa katika Shamba la Edeni. Magonjwa ya kimwili na hata kifo ni sehemu ya maisha haya na hayawesi kuondolewa kabisa maishani haya. Wakati mwingine watu wa Mungu huwa wagonjwa kutokana na mambo ya maumbile au hali zao za kimwili. Lakini haijalishi kifo kimetokana na nini, hiyo ndio njia ya sisi kuingia katika uzima wa milele na Mungu.

Shetani anaweza kumletea mtu mateso kama vile alivyomfanya Ayubu; lakini kila kitu ambacho Shetani atakiguza maishani mwetu ni lazima kwanza apitie kwa Mungu. Pia ni kweli kwamba Mungu anaweza kusababisha au kuruhusu ugonjwa kuingia miilini mwetu. Je, si ni kweli kwamba wakati wa mateso ndipo tunastahili kumkaribia Mungu. Hata katika wakati huo wa mateso tunaweza kujikabidhi mikononi mwake bila woga huku tukijua kwamba Yeye atafanya kile ambacho kinatufaa zaidi.

Katika Yohana 9:1-11 Yesu alimponya mtu ambaye alikuwa kipofu tangu kuzaliwa kwake. Nao wanafunzi wake wakamuuliza, "Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu? Yesu akajibu, "Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake."

Wakati mwingi Mungu huleta matokeo mazuri ya kiroho maishani mwetu kuptitia kwa magonjwa sio tu kwa mhusika bali pia kwa watu wanaomzunguka. Nayo 2 Wakorintho 4:15-17 inasema kuhusiana na swala hili kwa njia ya wazi kabisa: "Kwa maana mambo yote ni kwa ajili yenu, ili neema hiyo ikiongezwa sana, kwa hao walio wengi shukrani izidishwe, na Mungu atukuzwe. Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanya utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana."

Je, "kumwamini Bwana" ni kusema kwamba mtu hatatafuta matibabu ya madaktari?

Maandiko yanafundisha kwamba uponyaji wa kiungu ni mweke na baraka ya wana wa Mungu. Pia yanafundisha kwamba ili kumpendeza Mungu hatuna budi tuwe na imani. Lakini watu wengi huambatanisha imani na uponyaji wa kimwili tu. Lakini huku ni kupotoka Maandiko. Imani huguza kile sehemu ya maisha yetu na pia inahusiana zaidi na uhusiano wetu na Mungu kuliko yale ambayo tutatenda au kutotenda kuhusu matibabu.

Warumi 14:22-23 inasema, "Ile imani uliyo nayo uwe nayo nafsi mwako mbele za Mungu. Heri mtu yule asiyejihukumu nafsi yake katika neno lile analolikubali. Lakini aliye na shaka, kama akila, amehukumiwa kuwa ana hatia, kwa maana hakula kwa imani. Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi."

Kuna maswala ambayo Biblia haineni wazi wazi na ni makosa kwetu kujaribu kujaza pengo hizo kwa manufaa ya watu wale wengine. Kuna viwango tofauti vya imani, hii ni kumaanisha kwamba Mungu anaweza kuhuisha na kuongoza watu kwa njia tofauti tofauti na pia kwa njia tofauti katika muktadha tofauti tofauti. Hata ingawa watakatifu wametumia madaktari kwa njia moja au nyingine na wakaendelea kudumisha imani yao, kuna nyakati nyingi ambapo imani na mwongozo wa kibinasi humfanya mtu kujitenga na madawa na matabibu. Lakini swala hili la matumizi ya madawa halihitaji kuwa limetokana na msukumo wa watu wale wengine, bali linahitaji kutokana na uamuza wa mtu binafsi kulingana na imani yake. Lililo la muhimu zaidi ni sisi kuweka tumaini na ujasiri wetu kwa Bwana. Na ni jambo muhimu sisi kumtumaini Bwana na kuwa na ujasiri kwake. Tunahitaji kumtafuta Mungu na kunyenyeka kwa mapenzi na makusudi yake iwe ni katika hali ya mateso au katika hali ya afya nzuri. "Bwana twaomba utuongezee imani yetu!"



JE, WAJUA?

Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, ... mtukuzeni Mungu katika mili yenu. —1 Wakorintho 6:19-20

Ulaji wa vyakula visivyofaa na magonjwa yanayotokana na watu kuwa wanene sana kwa ajili ya kula kupita kiasi ni jambo ambalo linasababisha watu karibu 678,000 kufa kila mwaka katika nchi ya Marekani. Katika miaka 30 iliyopita idadi ya watu wazima wenye miili mikubwa katika nchi hiyo imezidi maradufu, ilhalii kati ya watoto idadi hiyo imekua mara tatu, na ikaongezeka mara nne kati ya vijana walibalehe (cspinet.org).

Basi mtoto wa Mungu anahitaji kutambua kwamba mwili wake ni hekalu la Mungu na kuutunza kwa kufuata tabia zinazofaa na zitakazomletea afya nzuri, kwa njia ya kula chakula kinachofaa, na pia kwa kufanya mazoezi.



KATIKA JINA LA YESU

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Lakini Petro akasema, Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende. — Matendo 3:6

Wakati kiwete ambaye alikuwa katika lango la hekalu alipomtazama Petro na Yohana huku akitarajia msaada wa kifedha wao walimsimamisha katika jina la Yesu, na mtu huyo akapata kuponywa kwa njia ya kiungu. Watu wakashangaa. Naye Petro akawaambia kwamba sio kwa kupitia kwa nguvu au utakatifu wao ndipo mtu huyo akaweza kutembea; “imani ile iliyo kwake ye ye imempatia huyu uzima.” Uponyaji ulipatikana kuitia kwa imani katika jina la Yesu.

Hata katika siku zetu kungali kuna nguvu katika jina la Yesu ambalo lina uwezo, ni la ajabu, na ni lenye kupendeza. Wakati mwingi sisi humaliza maombi yetu kwa kusema: “Kwa jina la Yesu.” Kwa kweli hiyo ni njia inayofaa ya kumalizia maombi, lakini nguvu katika jina la Yesu ndio moyo na msingi wa kumtafuta Mungu ili aingilie kati, na sio tu njia ya kumaliza maombi. Hakuna jina lingine chini ya mbingu lililo kama jina la Yesu. Wakati tunaliitia jina hilo sisi huwa tunaliitia jina la yule ambaye ni muumbaji wa wanadamu, mwokozi wa ulimwengu, kichwa cha kanisa, Mfalme wa Wafalme, Bwana wa Mabwana, alfa na omega, mwanzo na mwisho.



Shetani anachukia jina la Yesu na akilisikia ye ye hutetemeka. Roho chafu hazina budi kutoroka wakati watu watakatifu wanaliitia jina hilo. Tunaweza kukabiliana na nguvu za uovu kwa ujasiri, tukakabiliana na mateso kwa ujasiri, na kushughulikia giza la ulimwengu kwa tumani, kwa maana tunaweza kumkaribia ye ye ambaye alishinda maadui zote, akashinda hata kifo. Sisi wahudumu na wafanyi kazi wa injili hatuna haja ya kuogopa kufeli au kukosa matokeo ya kazi yetu. Nguvu za uponyaji na neema ya kumdumisha mtu sio yetu bali ni ya Mungu. Basi tumwachie Mungu matokeo ya maombi yetu.

Yesu ndiye mwanzilishi na mkamilishi wa imani yetu. Ombi letu ni kwamba imani na tumaini letu lipate uhai mpya wakati ambapo tunawaombea watu ambaa wamefungwa na kugandamizwa na dhambi. Tunaweza kuomba kwa mamlaka na ujasiri wakati tunapoomba kwa jina la Yesu. Wakati wagonjwa na watu wengine wanaoteseka wanahitaji msaada wa dharura tunaweza kumtafuta Mungu kwa uhakika kuitia kwa mwana wake mpendwa. Hata ingawa sisi ni wanadamu wenye udhaifu wa uwanadamu lakini kwa sababu sisi ni wana wa Mungu tunazo nguvu katika jina la Yesu. ■